GRADE 5 END OF YEAR EXAMS

KISWAHILI

Time: 1Hour

Soma makala yafuatayo halafu ujibu maswali yanayofuata.



Katika msitu wa Eshikalame, Njiwa alijulikana sana kwa sauti yake ya kupendeza. Karibu kila mnyama na kiumbe katika msitu huo alimfahamu kwa ushauri wake aliowatolea. Kila wakati wa jua kuaga miti, ungewapata ndege wakiwa wamejaa kwenye mti ili kufurahia utamu wa nyimbo na ushauri wa njiwa. Wanyama mbalimbali pia walisimama chini ya mti huo. Siku moja, palitokea vita katika msitu huo. Wanyama na ndege walipigana bila kujali. Walipokuwa katika hali hiyo ya vita, Njiwa aliwakariria shairi lililofanya kuacha kupigana. Alianza hivi:

Na wenzangu sikiliza, vita ni kitu kibaya,
Wengi wetu angamiza, kuua bila ya haya,

Kwa makini kichunguza, hapakuwa na ubaya,
Sote tuweni pamoja, tuwe na amani tena.

Makosa yakitokea, usamehe tafadhali,
Vyema wewe kutulia, hasira naziwe mbali,
Jamani nakuambia, yote haya ni ukweli,
Sote tuweni pamoja, tuwe na amani tena.

1. Kulingana na makala haya, Njiwa;
    A. alijua karibu kila mnyama na kiumbe.
    B. alijulikana na kila mnyama na kiumbe.
    C. alijulikana na wanyama na viumbe wengi.
    D. alikuwa akitolewa ushauri.